TANGAZO LA SERIKALI Na. 23 la tarehe 20/1/2023

SHERIA YA USIMAMIZI WA HAKI NA MATUMIZI YA SHERIA,
(SURA YA 358)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 4)*

KANUNI ZA UTARATIBU WA KUHAMISHA NA KUSIMAMIA MASHAURI YALIYOPANGWA KWA HAKIMU MWENYE MAMLAKA YA NYONGEZA ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
USIMAMIZI WA MASHAURI

4. Amri ya kuhamisha shauri.
5. Rejesta na utunzaji.
6. Majukumu ya Msajili.
7. Usajili baada ya amri ya kuhamisha.
8. Uchukuaji wa kiri na usikilizwaji wa shauri.
9. Rufaa na mambo mengine.
10. Kushindwa kumaliza shauri.
11. Kuitisha shauri lililohamishwa.
12. Sehemu ya kusikilizia shauri.

SEHEMU YA TATU
MAOMBI

13. Mahali pa kufungua maombi.

14. Usikilizwaji wa maombi.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI MENGINEYO

15. Mahali pa kuwasilisha indhari ya rufaa.
16. Kutolewa kwa kumbukumbu ya rufaa, nakala ya mwenendo na uthibitisho wa ucheleweshwaji.
17. Gharama.

MAJEDWALI

SHERIA YA USIMAMIZI WA HAKI NA MATUMIZI YA SHERIA,
(SURA YA 358)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 4)*

KANUNI ZA UTARATIBU WA KUHAMISHA NA KUSIMAMIA MASHAURI YALIYOPANGWA KWA HAKIMU MWENYE MAMLAKA YA NYONGEZA ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Utaratibu Kuhamisha na Kusimamia Mashauri Yaliyopangwa kwa Hakimu mwenye Mamlaka ya Nyongeza za Mwaka 2023.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitasimamia utaratibu wa kuhamisha mashauri kutoka Mahakama Kuu kwenda kwa hakimu na usimamizi wa mashauri hayo.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 237

"Jaji Mfawidhi" ina maana sawa na iliyotolewa chini ya Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, na inajumuisha Kaimu Jaji Mfawidhi;

"hakimu" maana yake ni hakimu mkazi mwenye mamlaka ya nyongeza; na

"Msajili" maana yake ni Msajili wa Mahakama Kuu, Naibu Msajili na Kaimu Naibu Msajili.

## SHEMU YA PILI
## USIMAMIZI WA MASHAURI

Amri ya kuhamisha shauri

4.-(1) Uhamishaji wa shauri lolote kutoka Mahakama Kuu kwenda kwa hakimu utakuwa kwa njia ya amri ya kuhamisha shauri itakayotolewa, kusainiwa na kuwekwa tarehe na Jaji Mfawidhi.

(2) Amri ya kuhamisha shauri chini ya kanuni ndogo ya (1) itafanywa-

(a) katika shauri la jinai linalosikilizwa na Mahakama Kuu katika mamlaka ya awali, baada ya kumkabidhi mshtakiwa Mahakama Kuu kwa usikilizwaji, na kabla ya kuchukuliwa kwa kiri; na
(b) katika mashauri mengine, baada ya kumbukumbu kukamilika, na kabla Mahakama Kuu haijaanza kusikiliza shauri linalokusudiwa kuhamishwa.

(3) Amri ya kuhamisha shauri chini ya kanuni hii itaainisha-

(a) maelezo ya shauri linalokusudiwa kuhamishwa;
(b) jina la hakimu ambaye shauri linahamishiwa kwake; na
(c) jina la mahakama ya hakimu mkazi ambapo shauri lililohamishwa litasikilizwa.

(4) Amri ya kuhamisha shauri chini ya kanuni hii itashabihiana kwa kadiri inavyowezekana na Fomu A iliyoanishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Rejesta na utunzaji

5.-(1) Kutakuwa na rejesta kadhaa ambamo kutaingizwa maelezo ya mashauri yaliyohamishiwa kwa hakimu.

(2) Rejesta chini ya kanuni hii zitatunzwa na Msajili.

(3) Kutakuwa na muhuri wa mahakama inayoendeshwa na hakimu kama ulivyoanishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi ambao utatunzwa na msajili.

Majukumu ya Msajili

6.-(1) Msajili atatekeleza majukumu yote yanayohusiana na mashauri yaliyohamishiwa kwa hakimu

kana kwamba mashauri hayo yapo Mahakama Kuu.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kanuni ndogo (1), Msajili atatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kuandaa ratiba ya mashauri pale inapobidi;

(b) kukadiria gharama za mashauri;

(c) kutekeleza tuzo na amri;

(d) kuandaa takwimu;

(e) kuhuisha mashauri katika mfumo wa usimamizi wa mashauri na rejesta;

(f) kuidhinisha nyaraka; na

(g) kuwa mtunzaji wa mwisho wa kumbukumbu.

Usajili baada ya amri ya kuhamisha

7.-(1) Baada ya kutolewa kwa amri ya kuhamisha shauri, Msajili ataingiza taarifa za shauri lililohamishwa katika rejesta chini ya Kanuni hizi na kusababisha shauri kupelekwa kwa hakimu.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kanuni hii, taarifa zitakazoingizwa kwenye rejesta zitajumuisha-

(a) namba ya shauri baada ya kuhamishwa;

(b) maelezo ya wahusika;

(c) namba ya shauri la Mahakama Kuu;

(d) namba ya shauri asilia au la ukabidhi;

(e) jina la hakimu aliyepangiwa;

(f) tarehe ya amri ya kuhamishwa; na

(g) uamuzi na tarehe yake.

Uchukuaji wa kiri na usikilizwaji

8.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, hakimu ambaye amepangiwa shauri, atachukua kiri mara baada ya shauri kuhamishwa.

(2) Baada ya kuchukua kiri chini ya kanuni ndogo ya (1), hakimu atasikiliza shauri hadi mwisho kwa tarehe itakayopangwa na Msajili au tarehe nyingine baada ya hapo.

Rufaa na mambo mengine

9.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, hakimu ambaye amepangiwa shauri la rufaa au shauri lingine lolote, atasikiliza shauri mara baada ya shauri

kuhamishwa.

(2) Baada ya kupokea amri ya kuhamisha shauri na kumbukumbu ya rufaa au shauri lingine lolote lililotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1), hakimu atapanga tarehe bila kuchelewa, na kwa tarehe itakayopangwa, atasikiliza shauri kwa mfululizo hadi kumalizika au, kwa sababu zitakazoandikwa, ataliahirisha hadi tarehe nyingine.

Kushindwa kumaliza shauri.

10.-(1) Endapo hakimu atashindwa kuendelea na usikilizwaji wa shauri asilia, rufaa au shauri lingine lolote, kwa sababu ya kifo, ugonjwa au sababu yoyote ya msingi, Jaji Mfawidhi, kwa amri atakayoweka saini, atapanga upya shauri kwa hakimu mwingine ili kuendelea na usikilizaji.

(2) Hakimu anayepokea shauri chini ya kanuni hii, ataandika sababu za kupokea shauri na kuwajulisha wahusika wa shauri.

(3) Amri ya kupangwa upya kwa shauri chini ya kanuni hii itashabihiana kwa kadiri inavyowezekana na Fomu B iliyoanishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Kuitisha shauri lilohamishwa

11. Jaji Mfawidhi, kwa sababu za kipekee zitakazoandikwa, anaweza kuitisha shauri lililohamishiwa kwa hakimu-

(a) iwapo ni shauri la jinai, kabla ya kiri haijachukuliwa; na
(b) iwapo ni shauri linguine lolote, kabla ya kuanza kusikilizwa,

na katika mazingira hayo, shauri litaendelea Mahakama Kuu.

Sehemu ya kusikilizia shauri

12.-(1) Hakimu atasikilizia shauri katika eneo ambalo mahakama iliyotajwa katika amri ya kuhamisha shauri kwa kawaida huketi.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), kwa ridhaa ya Jaji Mfawidhi, hakimu anaweza kusikilizia shauri mahali pengine popote ndani ya eneo la mamlaka ya mahakama iliyotajwa katika amri ya uhamishaji na wahusika watajulishwa sehemu hiyo ya kusikilizia shauri.

## SEHEMU YA TATU
## MAOMBI

Mahali pa kufungua maombi

13.-(1) Maombi yanayotokana na mashauri yaliyohamishiwa kwa hakimu, yanayofunguliwa kabla au baada ya shauri lililohamishwa kuamuliwa, yatafunguliwa katika Mahakama Kuu.

(2) Baada ya kusajiliwa kwa maombi yaliyofunguliwa chini ya kanuni ndogo ya (1), Jaji Mfawidhi atatoa amri ya kuhamisha maombi inayoshabihiana kwa kadiri inavyowezekana na Fomu C iliyoanishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(3) Bila kujali masharti ya Kanuni hizi na kwa kuzingatia masharti ya Sheria nyingine yoyote, maombi ya ukadiriaji gharama na utekelezaji wa maamuzi yanayotokana na utekelezaji wa mamlaka ya nyongeza yatasikilizwa na Msajili.

(4) Kanuni hii haitamzuia hakimu kuamua na kutekeleza malipo ya gharama zilizoamriwa kulipwa wakati shauri linaendelea.

Usikilizwaji wa maombi

14. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi au sheria nyingine yoyote, maombi yanayotokana na shauri lolote lililoamuliwa na hakimu yatasikilizwa na hakimu aliyeamua shauri husika au hakimu mwingine yeyote atakayepangiwa.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MENGINEYO

Mahali pa kuwasilisha indhari ya rufaa
Sura ya 141

15. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Rufaa au sheria nyingine yoyote, indhari ya rufaa dhidi ya uamuzi wa mahakama ya chini inayotekeleza mamlaka ya nyongeza, itawasilishwa Mahakama Kuu.

Kutolewa kwa kumbukumbu ya rufaa, nakala ya mwenendo na uthibitisho wa ucheleweshwaji
Sura ya 141

16. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Rufaa au sheria nyingine yoyote, msajili ataandaa, kutoa na kupeleka kumbukumbu ya rufaa, nakala ya mwenendo na uthibitisho wa ucheleweshwaji kwa masuala yanayotokana na uamuzi wa hakimu.

Gharama

17. Kwa kuzingatia masharti ya sheria yoyote, uendeshaji wa mashauri mbele ya hakimu utagharimiwa na Mahakama Kuu.

FOMU A

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(4), 10(3) na 3(2)*

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 4(4))*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

INAYOKETI……………………

AMRI YA KUHAMISHA SHAURI

Shauri la Kikao cha Jinai/Rufaa ya Jinai /Rufaa ya Madai/Rufaa ya Ardhi/Maombi ya Mapitio/ (au shauri jingine lolote) Na……la Mwaka 20.… *(weka aina na namba ya shauri la Mahakama Kuu litakalohamishiwa kwa hakimu mkazi mwenye mamlaka ya nyongeza)*
Shauri asilia la ukabidhi/Shauri la Jinai/Shauri la Madai (au Shauri lolote la awali) Na…...la Mwaka 20.... (*ingiza aina na namba ya shauri la mahakama ya chini iliyopelekea shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa*) ya Mahakama ya Wilaya/Mahakama ya Hakimu Mkazi ya……..inayoketi………. (*weka jina na mahali inapoketi mahakama ya chini iliyosikiliza shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa*)

………………………. JAMHURI/MRUFANI/MWOMBAJI

*DHIDI YA*
……………………...MSHTAKIWA/MJIBU MAOMBI

*(weka maelezo ya wahusika katika shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa)*

AMRI YA KUHAMISHA
(*chini ya kifungu cha…. cha…….*)
*(weka kifungu cha Sheria kinachoruhusu kuhamisha shauri kwenda kwa hakimu mkazi mwenye mamlaka ya nyongeza)*

Inaamriwa kuwa Shauri la Kikao cha Jinai/Rufaa ya Jinai/Rufaa ya Madai/Rufaa ya Ardhi/Maombi ya Mapitio (au shauri lingine lolote) Na………… la Mwaka 20…… baina ya………………na…………………. linalotokana na uamuzi wa …………. (*weka jina la hakimu ambaye uamuzi wake unapingwa*) katika…………… *(weka maelezo ya shauri asilia*) la………………. (*weka maelezo ya mahakama asilia*) linahamishwa kwenda kusikilizwa na kuamuliwa na ………………………., hakimu mkazi mwenye mamlaka ya nyongeza.

Inaamriwa pia kwamba usikilizwaji wa shauri tajwa utafanyika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya …….………….

………………………..
Jaji Mfawidhi
Tarehe……….mwezi………………mwaka 20.…

FOMU B

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 10(3))*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
INAYOKETI……………………

AMRI YA KUPANGWA UPYA KWA SHAURI

Shauri la Kikao cha Jinai katika Mamlaka ya Nyongeza/Rufaa ya Jinai/Rufaa ya Madai/Rufaa ya Ardhi/Maombi ya mapitio (au shauri lingine lolote) Na……la Mwaka 20.……... *(weka namba ya shauri la mamlaka ya nyongeza)*
Shauri asilia la ukabidhi/Shauri la Jinai/Shauri la Madai (au shauri lingine lolote asilia) Na…… la mwaka 20.... (*weka aina na namba ya shauri la mahakama ya chini iliyopelekea shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa*) la Mahakama ya Wilaya/Mahakama ya Hakimu Mkazi ya……..inayoketi………. (*weka jina na mahali inapoketi mahakama ya chini iliyosikiliza shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa*).

………………………. JAMHURI/MRUFANI/MWOMBAJI

*DHIDI YA*

……………………...MSHTAKIWA/MJIBU MAOMBI

(weka maelezo ya wahusika wa shauri linalopangwa upya)

AMRI YA KUPANGWA UPYA KWA SHAURI
*(Chini ya kifungu cha……. cha…….)*

*(weka kifungu cha Sheria kinachoruhusu kupangwa upya kwa shauri kwa hakimu mkazi mwenye mamlaka ya nyongeza)*

Inaamriwa kuwa Shauri la Kikao cha Jinai la Mamlaka ya Nyongeza/Rufaa ya Jinai/Rufaa ya Madai/Rufaa ya Ardhi/Maombi ya Mapitio/ (au shauri lingine lolote) Na…… la mwaka 20…… baina ya…………………na……….…….hapo awali mbele ya……………………...*(weka jina la hakimu wa awali ambaye hakuweza kumaliza usikilizwaji)* limepangwa upya kwa ajili ya kusikilizwa na ………………………., hakimu mkazi mwenye mamlaka ya nyongeza.

Inaamriwa pia kwamba usikilizwaji wa shauri tajwa utafanyika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya …….…………….

………………………..
Jaji Mfawidhi
Tarehe……….mwezi………………mwaka 20.….

FOMU C

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 13(2))*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

INAYOKETI……………………

AMRI YA KUHAMISHA SHAURI LA MAOMBI

Maombi ya Jinai/Madai Na……la Mwaka 20.… *(weka namba ya shauri la maombi la Mahakama Kuu litakalohamishiwa kwa hakimu mkazi mwenye mamlaka ya nyongeza)*
Yanayotokana na Shauri la Kikao cha Jinai/Rufaa ya Jinai/Rufaa ya Madai/Rufaa ya Ardhi (au Shauri lolote linalohamishika) Na…...la Mwaka 20.... (*weka aina na namba ya shauri la mahakama ya chini iliyopelekea shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa*) ya Mahakama Kuu/Mahakama ya Hakimu Mkazi ya……..inayoketi……….(*weka jina na mahali inapoketi mahakama ya chini iliyosikiliza shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa*).

………………………. MWOMBAJI

*DHIDI YA*

……………………...MJIBU MAOMBI

*(weka maelezo ya wahusika katika maombi litakalohamishwa)*

AMRI YA KUHAMISHA

*(Chini ya kanuni ya 13(2) ya Kanuni za Utaratibu Kuhamisha na Kusimamia Mashauri Yaliyopangwa kwa Hakimu mwenye Mamlaka ya Nyongeza za Mwaka 2022.)*

Inaamriwa kuwa Maombi ya Jinai/Madai Na……la Mwaka 20.…baina ya………………na…………………. Yanayotokana na Shauri la Kikao cha Jinai/Rufaa ya Jinai/Rufaa ya Madai/Rufaa ya Ardhi (au Shauri lolote linalohamishika) Na…...la Mwaka 20.... (*weka aina na namba ya shauri la mahakama ya chini iliyopelekea shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa*) ya Mahakama Kuu/Mahakama ya Hakimu Mkazi ya................……..inayoketi…….......(*weka jina na mahali inapoketi mahakama ya chini iliyosikiliza shauri la Mahakama Kuu linalohamishwa*) linahamishwa kwenda kusikilizwa na ………………………., hakimu mkazi mwenye mamlaka ya nyongeza.

Inaamriwa pia kwamba usikilizwaji wa shauri tajwa utafanyika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya ……….……….

………………………..
Jaji Mfawidhi
Tarehe……….mwezi………………mwaka 20.….

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(3))*

MUHURI WA MAHAKAMA




Dar es Salaam,
9 Januari, 2023

IBRAHIM HAMIS JUMA,
*Jaji Mkuu*